**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 Certified**

Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali


## TAARIFA KWA WAZALISHAJI, WAINGIZAJI, WASAMBAZAJI NA WAUZAJI WA MAZIWA MBADALA YA WATOTO (*INFANT FORMULA* NA *FOLLOW UP FORMULA*)

**Dar es Salaam, 14 Februari, 2023**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuwakumbusha wazalishaji, waingizaji, wasambazaji na wauzaji wa bidhaa za chakula ikiwemo maziwa mbadala ya watoto kuzingatia matakwa ya viwango na kuhakikisha zinasajiliwa na TBS kabla ya kuletwa nchini.

Kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Sura 130, bidhaa zote za chakula ikiwa ni pamoja na maziwa mbadala ya watoto yanayozalishwa nchini au yanayotoka nje ya nchi hutakiwa kuthibitishwa ubora na usalama wake kabla ya kuruhusiwa kusambazwa au kuuzwa.

Vilevile, kwa mujibu wa *The Standard (Import Registration and Batch Certification) Regulation, 2021* pamoja na EAS 4-1 & 2:2021 (*Infant formula –specifications*) taarifa za lebo (labelling information) za bidhaa za maziwa mbadala ya watoto zinatakiwa kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa pamoja. Aidha taarifa hizo hazitakiwi kuwa na picha au michoro ya aina yoyote inayoonesha mtoto au mwanamke au zinazohamasisha matumizi ya maziwa mbadala ya watoto isipokuwa ile inayoonesha namna ya kuandaa/kutayarisha maziwa hayo.

Lengo la matakwa hayo hapo juu ni kuwezesha matumizi sahihi na kuepuka athari zinazoweza kujitokeza kutokana na kutokuzingatia kikamilifu maelekezo yanayoandikwa kwenye kifungashio vilevile, kutoathiri jitihada za unyonyeshaji wa maziwa ya mama.

Shirika litaendelea kuhakikisha kuwa matakwa ya Sheria kuhusiana na ubora na usalama wa bidhaa zote zikiwamo maziwa mbadala ya watoto yanazingatiwa ili kumlinda mlaji.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800 110 827**.

Imetolewa na:

Gladness H. Kaseka
**Meneja wa Uhusiano na Masoko**


**TBS HEADQUARTERS**
Physical Address
Tanzania Bureau of Standards
Ubungo, Morogoro Road /
Sam Nujoma Road
P. O. Box 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Tel. No: +255 22 245 0298/
+255 22 245 0206
Telefax: +255 22 2450959
Hotline: 0800110827
E-mail: info@tbs.go.tz
Website: http://www.tbs.go.tz
E-mail address for customer complaints:
complaints@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS CENTRAL ZONE**
Physical Address
Kambarage Tower
P.O. Box 2956
DODOMA,
TANZANIA
Tel. No:
+255 26 2520310

**TBS LAKE ZONE**
Physical Address
NSSF Building,
3rd Floor
P.O. Box 1814
MWANZA,
TANZANIA
Tel. No:
+255 28 2501127

**TBS NORTHERN ZONE**
Physical Address
NSSF Mafao House
Building, 2nd Floor
P.O. Box 2399
ARUSHA,
TANZANIA
Tel. No:
+255 27 2520143

**TBS SOUTHERN HIGHLANDS ZONE**
Physical Address
NHIF Building,
7th Floor
P.O. Box 1674
MBEYA,
TANZANIA
Tel No:
+255 25 2502848

**TBS SOUTHERN ZONE**
Physical Address
MTUWASA Building
P. O. Box 1396
MTWARA,
TANZANIA
Tel. No:
+255 23 2334477

**TBS WESTERN ZONE**
Physical Address
NSSF Building (Mafao House), 2nd Floor
P. O. Box 1276
KIGOMA,
TANZANIA
Tel. No:
+255 28 2804023